SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.18 June 2026

MAKOSA YA LUGHAWIYA YANAYOJITOKEZA KATIKA MAANDISHI YA WANAFUNZI WANAOJIFUNZA KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

Miza Vuai Kombo
mizavuali7@gmail.com
Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
Haroun Ayoub Maalim
Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
Kijakazi Omar Makame
Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar

Received: October 20225, Accepted: December 2025, published June 2026
© SUMAIT University Journal 2026

Abstract:

This article examines how the complexity of language skills triggers linguistic errors in writing among Kiswahili learners at the State University of Zanzibar. The examples analyzed are drawn from unacceptable errors in writing. The data for this article were collected and analyzed through the theory of language competence. Data were gathered through text analysis. Among the errors identified in students are mistakes in noun class categorization, grammatical agreement errors, lack of cohesion, lexical errors, near-negation, and the use of personal and singular/plural affixes. This article is expected to contribute to academic resources in teaching Kiswahili as a foreign language. Furthermore, Kiswahili teachers for non-native learners will be able to identify the challenges facing their students and provide solutions, thereby enabling more effective teaching.

Ikisiri

Makala hii imechunguza ugumu wa stadi ya kuandika unavyoibua makosa ya kilughawiya katika maandishi kwa wanafunzi wa Kiswahili kwa wageni kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mifano iliyochambuliwa ni kutoka makosa yasiyostahamilika katika uandishi. Data za Makala hii zimekusanywa na kuchambuliwa kupitia nadharia ya umilisi wa lugha. Data zimekusanywa kupitia

uchanganuzi matini. Miongoni mwa makosa yaliyobainika kwa wanafunzi ni pamoja na makosa ya uainishaji wa ngeli za majina, makosa katika upatanishi wa kisarufi, kukosekana kwa ushikamani, kosa la kimsamiati, ukanushi wa karibu, matumizi ya viambishi nafsi na viambishi vya umoja na wingi. Makala hii inatarajiwa kuongeza nyaraka za kitaaluma katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni. Aidha, walimu wa Kiswahili kwa wageni watabaini changamoto zinazowakumba wanafunzi wao na kuzitolea suluhisho ili waweze kufundisha kwa ufanisi zaidi.

Keywords: Lughawiya, stadi ya kuandika, stadi ya kuzungumza, lugha ya pili, lugha ya kigeni,

1.0 Utangalizi

Stadi ya kuandika hurejelea uwezo wa mwanafunzi kuunda maandishi yenye mpangilio, mantiki na ufasaha kwa kutumia kanuni za lugha kwa usahihi, ikiwa ni mchakato unaojumuisha upangaji wa mawazo, uundaji wa rasimu, uhariri na uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa. Kwa mujibu wa **[3]** kuandika ni mchakato tata wa kiakili unaohusisha upangaji, uandishi na marekebisho ya maandishi kulingana na malengo ya mwandishi; huku **[4]** akisisitiza umuhimu wa kujifunza kwa vitendo ambapo mwanafunzi hujenga ujuzi kupitia mazoezi endelevu. Aidha, **[4]** anaeleza kuwa kuandika ni stadi ya kijamii inayoathiriwa na muktadha, hadhira na madhumuni yamawasiliano, hivyo mwanafunzi huhitaji kuelewa kanuni za kiutamaduni, kisarufi na kimaandishi za lugha anayojifunza ili kufanikisha uandishi wenye ufanisi.

Lughawiya ni sayansi ya lugha katika matawi manne makuu ya lugha. Matawi hujitokeza katika stadi ya kuandika na kuzungumza. Kutokana muktadha wa Makala hii, stadi ya kuandika ndio iliyochanganuliwa kwa kutazama mofolojia, sintaksia, na semantikia. Matawi hayo ndio huitambulisha lugha kisayansi. Mchakato wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili au lugha ya kigeni huegemea matawi hayo kwa kupima uwepo wa stadi za lugha kama vile kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza. Hivyo, kusoma na kusikiliza ni stadi za kupokea na kuzungumza na kuandika ni stadi za kutoa **[9]** wanafunzi wa lugha ya pili wanajifunza lugha kwa lengo la kufikia uwezo wa kumudu stadi zote za lugha. **[2]** ameeleza stadi ya kuzungumza ni moja kati ya stadi nne kuu za ujifunzaji wa lugha. Mambo yanayoathiri stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya kigeni mionngoni mwao ni kuona aibu katika kufanya mazoezi, uchache wa misamiati ya lugha wanayojifunza na mwisho kukosa mwamko katika ujifunzaji. Aidha, wanafunzi watakaofanya mazoezi mengi kwa namna tafauti, ikiwemo kusikiliza vyombo vya habari, au kutumia kamusi kwa muda mwingi itamasaidia kujifunza lugha kwa ufanisi.

[12] ameangalia zaidi mambo yanayoathiri upataji wa stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa sekondari mashariki ya Turkana nchini Kenya. Mtafiti amebaini kuwa walimu wengi wanafundisha kwa kutumia vitabu vya ziada, vitabu vya kiada chaki na ubao, kama ni vifaa muhimu vya ufundishaji darasani na kuendelea kusema walimu wachache tu ndio wanaotumia mbinu shirikishi darasani. Hata hivyo, mbinu ya michezo ndani ya darasa inapingwa na walimu wengi kwa sababu inapoteza muda, aliendelea zaidi kwa kusema, walimu walio wengi hawatumii muda mwingi

kutoa mazoezi darasani. Pia, anashauri kwamba ili mwanafunzi apate stadi ya kuzungumza ipasavyo, ni lazima mwalimu atumie vifaa vya kisasa katika ufundishaji wake.

Katika kuchunguza ugumu na ubaya wa stadi ya kuzungumza, Sebazungu na **[9]** anasema, mambo yanayopelekea stadi ya kuzungumza kuwa mbaya katika skuli za sekondari za Kicukiro nchini Rwanda ni kujisikia aibu kwa wanafunzi wakati wa kuzungumza Kiswahili, Wanafunzi kukosa hamasa wakati wa kujifunza lugha,wanafunzi kujisikia hofu wakati wa kuzungumza kwenywe kundi la watu, ukosefu wa misamiati ya kutosha, kukosa kujiamini wakati wa kuzungumza lugha, mwisho mtafiti alijaribu kuweka mapendekezo yake kwa kushauri, wizara ya elimu ya nchini Rwanda iweke vifaa vya kutosha katika kujifunza lugha maskulini, ushirikiano wa wazazi na walimu katika kujifunza lugha, na mwisho mwalimu awe na mikakati ya kutosha katika kumsaidia mwanafunzi kujifunza lugha. stadi ya kuandika kuwa ni hali ya kukuza lugha kwa kuelezea mawazo au hisia kwa njia ya maandishi Kuandika ni uwezo wa kunukuu ishara za lugha na kubuni mawasiliano kwa ishara hizo. Stadi hii huwawezesha wanafunzi kujifunza lugha kama stadi za msingi za kujifunza lugha.
[1] ameangalia zaidi kiwango cha ufanisi kati ya lugha ya Kiarabu na Lugha ya Kiingereza kwa walimu wanafunzi kupitia mtazamo wa mabadiliko katika stadi ya uandishi, katika chuo Cha Taiba, Madina Saudi Arabia, mtafiti amebaini walimu wanafunzi wanakabiliwa na mambo kama yafuatayo katika uandishi miongoni mwa mambo hayo ni ukosefu wa msamiati wa kutosha katika uandishi, sarufi kutokuwa sahihi, miundo ya sentensi inayokubalika, hamna ushikamani unaokubalika katika sentensi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mijengeko ya lugha zote inaonesha kwamba makosa yote ni sawa kwa upande wa uwandishi kupitia mazoezi ya nyumbani na mazoezi ya darasani.

[9] ameangalia zaidi mbinu za kufundishia zinavyochochea zaidi maendeleo katika lugha ya kingereza, nakugundua kuwa walimu walio wengi wanaofundisha stadi za lugha wanashindwa kubaguwa kulingana na muda na idadi ya wanafunzi darasani walimu wanatilia mkazo katika stadi ya kuandika na kusoma tu na kutenga stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Aliendelea kusema, walimu wanatumia mbinu ya muhadhara na kuacha kutumia mbinu shirikishi na akaendelea kwa kusema walimu wanatumia muda mchache tu kutumia mbinu shirikishi darasani.
[12] wameangalia zaidi vikwazo vya kusomesha stadi ya kuzungumza na kuandika nchini Bangladesh kwa darasa la mtandaoni. Mtafiti huyu amegundua kuwa walimu wengi kukosa mafunzo ya kutosha, hivyo kupelekea walimu kutofikia malengo yao ya ufundishaji. Mtafiti ametoa mapendekezo na kusema kuwa walimu wapewe mafunzo ya kutosha katika darasa la mtandaoni ili kukabiliana na changamoto wanazokabiliana nazo wakati wa kufundisha stadi za kuzungumza na kuandika.

2.0 Nadharia ya umahiri wa lugha.

Utafiti huu unajikita katika nadharia ya Umahiri wa lugha ya Chomsky, ambayo iliendelezwa na kutumiwa kama nadharia ya umahiri wa lugha ya Kiisimu na **[7]** Dhana hii ya umahiri wa lugha si ngeni, ilikuwepo tangu wanafonolojia walipoingia katika isimu karne ya kumi na nane (Chomsky 1957). Umahiri wa kiisimu katika lugha ni uwezo wa mtu binafsi kuelewa na kutumia vigezo vya kiisimu vinavyoshamiri matumizi ya lugha husika. Kutokana na maelezo haya ya **[4]** mtu huwa na

umahiri wa kiisimu katika lugha yoyote ikiwa ni mzaliwa wa lugha hiyo au ikiwa anajifunza kama Lg2.

[7] anaendelea kusema kuwa umahiri haupatikani tu katika lugha bali hupatikana katika taaluma nyingine kama vile; sosholojia na saikolojia. **[7]** akielezea nadharia yake ya umahiri wa kiisimu anaeleza kuwa umahiri hupatikana kupitia mazoezi na ujuzi. Pia anasema kuwa umahiri huu hupimwa kupitia mfumo maalum uliotengwa na wanajamii wa lugha husika, kama vile ufasaha katika mawasiliano ambao hupewa wasemaji wa lugha ili kupima umahiri wao wa kiisimu katika lugha husika.

Msingi wa nadharia hii unaona kuwa, umahiri wa kiisimu wa mtu hukuzwa na hali yake mwenyewe. Mtu anapozidi kufanya mazoezi katika lugha husika ndivyo ujuzi wake katika matumizi ya lugha hiyo huongezeka na kuimarika. Umahiri wa kiisimu katika lugha yoyote ile huambatanishwa na matumizi yake katika usemi au katika maandishi au kuelewa jinsi lugha hiyo inavyopangwa kisarufi na jinsi inavyoathiri maisha ya mtu. Mwanaisimu huyu **[4]** anahitimisha kwa kusema kuwa umahiri wa kiisimu huhusisha kila kitu kinachohusiana na lugha kama vile; muundo, mawasiliano na utendaji.

3.0 Makosa yaliyobainika kwa wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya kigeni

Kujifunza lugha ya pili ni mchakato mrefu unaokabiliwa na mambo mengi. Aidha, ugumu na changamoto hizo zinaweza kujitokeza kwa namna tofauti. Kupitia wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kumebainika matatizo kadhaa yasiyovumilika katika maandishi. Makosa haya yameitwa yasiyovumilika kiuwandishi kwa sababu yangeweza kuvumiliwa pindi yangejitokeza katika mazungumzo. Miongoni mwa makosa hayo ni:

3.1 Uainishaji wa Ngeli za Majina

Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni wanatatizika mno katika kujifunza kwao hasa katika upatanishi wa kisarufi. Katika stadi ya kuandika, utafiti wa Makala hii ulibaini matumizi ya ngeli kwenye maandishi lakini kuna idadi kubwa ya wanafunzi wanaoshindwa kutumia ngeli za maneno kwa usahihi. Kwa mfano uainishaji wa makundi ya ngeli za {a/wa} ndilo lililowatatiza wanafunzi wengi.

Wanafunzi wa tatu 03 kati ya watano 05 walishindwa kutumia kimilikishi mwafaka cha jina **<ng’ombe>** ambacho ni “-angu.” Majibu yao mengi yaliangukia katika muundo wa ***<ng’ombe yangu>.*** Badala ya ngombe wangu. Pia, kulikuwa na kundi wanafunzi wanne 04 walitatizika kupatanisha vizuri jina **<mama>** na kimilikishi **<ake>** vile vile, wanafunzi wawili 02 kati ya 05 walitatizika kupatanisha jina <**mwili**> na kimilikishi **<ake>** katika kundi la ngeli za {u/i}. Hivyo, majibu tuliyoyapata kutoka kwa wanafunzi waliofanya makosa haya ni kama ***<mama wake>, <mwili yake>*** na ***<mwili mke>*** **kitabu imepotea, ilipokuwa wanakwenda skuli kwa sababu njiani cheza sana**. Wanafunzi wanne kati ya watano walitatizika kupatanisha sentensi hii sawa na asilimia 80% Ngeli iliyoonekana kuwa rahisi katika kipengele hiki ni ile ya majina ya kundi la {ki/vi} kwani Maneno kama vile **< kisu, kiti, kipepeo>** waliyamudu wanafunzi wanne 04 kati ya 05.

Kwa ujumla haya yote yanahesabika kuwa ni makosa kutokana na misingi ya nadharia ya umilisi wa lugha, ambapo nadharia hii inahimiza mwanafunzi kuweza kumudu stadi zote nne za lugha. Hivyo

uainishaji wa ngeli hutegemewa ni kipengele cha kilughawiya kinachopimwa katika uandishi wa mwanafunzi. Hivyo kutokumudu miundo ya kisintaksia ni ishara ya kutokuwa na umilisi mzuri wa lugha husika. Mofolojia ni tawi la kiisimu linaloshughulikia miundo ya ndani au maumbo ya maneno. Hivyo wanafunzi hawawezi kugundua kwa urahishi miundo ya ndani ya lugha hadi pale watakapokuwa wamilisi na wabobevu wa lugha husika. Kwa sababu hiyo wanafunzi wanachotakiwa kuzingatia katika uainishaji wa upatanishi wa ngeli za majina ni viambishi awali vya nomino katika umoja na wingi ambapo wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya kigeni hushindwa kugundua kosa hilo. Hivyo, maelezo yanaonesha namna umilisi wa lugha unavyoweza kutatizika kupitia kuhusishwa kubainisha ngele za majina.

3.2 Upatanishi wa Kisarufi

Upatanishi wa kisarufi ni miongoni mwa makosa yanayoonekana dhahiri wakati wa maandishi. Kupitia kazi za wanafunzi wa chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar idara ya Kiswahili kwa wageni makosa hayo yanadhihirishwa kwa majibu yaliyotolewa na wanafunzi katika majibu waliyoyatoa kwenye karatasi za mazoezi walizopewa. Lengo kuu la mazoezi hayo lilikuwa kutathmini uwezo wao wa kupatanisha nomino na maneno mengine yanayoandamana na kutawaliwa nayo katika upatanishi wa kisarufi. Kwa mfano, neno <nanasi> kiingizi kioneshi cha karibu wanafunzi wanne 04 walikosa kati ya 05 na kusema **<nanasi hizi>** au **<nanasi hii>.** Pia Baadhi ya miundo potofu iliyotolewa na wanafunzi wengi ni kama mwili msafi, mwili safi, udevu urefu na udevu ndefu. Muundo wa nomino za kundi la {i/zi} kama vile nyumba uliwatatiza wanafunzi watatu 03 kati ya 05 waliokosa jibu sahihi kwa kutumia kiambishi mwafaka kwa kupatanisha jina hili na kivumishi refu. Pia wanafunzi wanne 04 kati ya 05 walishindwa kupatanisha jina koti na kivumishi zuri na badala yake walisema **<*koti lizuri*>**

Pia neno **< *mhandisi*>** wanafunzi watatu kati ya watano walishindwa kupachika kiambishi kioneshi cha karibu cha neno hilo. Baadhi ya wanafunzi walisema **<*mhandisi hii*>** na wengine **<mhandisi hizi>.** Hivyo walishindwa kusema mhandishi huyu. Kwa maana hiyo kanuni za kuandika zilionekana zinawashinda sana wanafunzi kwa sababu hawana umilisi wa lugha katika stadi ya kuandika. Hata hivyo, katika kanuni za kuzungumza wangeweza kuvumiliwa na kuonekana wanaweza kuzungumza hasa pale mwanafunzi aliposema **<*nanasi hizi*>** msikilizaji wa lugha mara nyingi hawezi kuona kuwa kuna makosa katika matamshi hayo kwa sababu lugha ya mazungumzo inayonafasi ya kuvumilia kwa baadhi ya makosa madogo kama hayo. Wataalamu kadhaa wamethibitisha kutokea kwa makosa ya upatanishi wa kisarufi.

[8] anasema kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hutumia ujumuishaji unaotokana na tajiriba ya mwanafunzi mwenyewe na huchukulia mazowea katika lugha zao na kupatanisha kupitia uzoefu wao wa kawaida na sio kufuata kanuni za lugha, ambapo wanafunzi wanaojifunza Kiswahili hutunga sentensi zenye makosa kwa kujumuisha kanuni za lugha ya pili. Katika hali hii, wanafunzi hutatizwa na majina kipofu, jiwe, ukuta, udevu, na mengine yanayokiuka utaratibu wa kawaida wa upatanishi wa nomino na kivumishi unaorejelea muundo wa kiambishi awali cha nomino katika kivumishi kinachoambatana nacho.

Pia anaonesha makosa mbalimbali wanayoyafanya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Anasisitiza kuwa wanafunzi wanashindwa kupatanisha matumizi ya neno mbuzi, kipofu, na mkulima, na . Hivyo, ni dhahiri kuwa wanafunzi hujirahisishia ujifunzaji kwa kujumuisha kanuni ya kuunda maneno kutokana na urahisi tu na sio kanuni (lughawiya) za lugha.

3.3 Kukosekama Kwa Ushikamani

Ushikamano ni dhana ya kipragmatik, ambayo hurejelea katika mtiririko wa habari au sentensi ili kuunda matini. Utafiti uliotokana na Makala hii umebaini kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili kwa wageni kama lugha yao ya kigeni wanakabiliwa na tatizo la ushikamani katika maandishi yao jambo linalofanya uonekane umahiri wa kuandika ni mgumu kuliko kuzungumza. Katika baadhi ya insha za wanafunzi tumebaini kushindwa na ushikamani wa neno na ushikamani wa sentensi.

> *Mwanafuzi X: Maisha katika Zanzibar ni nzuri, ninapenda kunywa juice ya sugercane katika forodani. Penye paka wengi ninapenda kucheza na paka na kupiga picha za paka*
> *Kila siku tangu jumatatu mpaka ijumaa. Huamka saa moja asubuhi, halafu mimi hunywa chai sa tangawizi na hukula matunda na mikate na chapati. Ninapenda majira sasa, Kwa hiyo mvua ndogo ndogo na hakuna jua kali*
> *Ninapenda kukaa ya bahari pia. Ahsante sana kwa maisha katika Zanzibar*.

Kipande hiki hakina ushikamani wa sarufi na mtiririko wa kimaana kwani kinachanganya mada tofauti tofauti bila uhusiano wa moja kwa moja kati ya sentensi. Pia, hakifuati mfululizo wa matukio au mawazo yanayoeleweka kwa urahisi.

> ***Mwanafunzi N*****:** Watu wa Zanzibar wanapenda watoto sana, waliamka kuhusu mvua na kucheza sana, ninapenda watoto wa kiembe samaki ni nzuri sana watoto wengi ni nzuri maskini hawana watoto familia yangu ninawatoto wanne. Lakini hapa marekani mimi ni peke yangu hamna kaka au dada pia wangeenda skuli kuanza nanaenda chekechea baadae hasa enda skuli ya msingi au ya sekondari. alijaribu kusoma kitabu cha fizikia lakini taa alizimika ghafla. Kesho ni siku ya kuzaliwa ya dada yangu, na ningependa kula keki ya chokoleti. Samaki kwenye soko alikuwa akining'inia kutoka kwenye ndoano.

Kipande hiki hakina ushikamani wa sentensi na maana kwa sababu sentensi haziungani au kuhusiana kwa namna yoyote ile. Mawazo yanaruka kutoka suala moja hadi jingine bila mpangilio au mfuatano wa kiamaana.

> ***Mwanafunzi Z*** *Hii ni mara yangu ya kwanza katika Afrika na katika Zanzibar. Hapa maisha na utamaduni ni tofauti sana na Italia, nchi yangu*
> *Nilifurahi kula ugali kwa mikono yangu, kitu chengine ninapenda hapa ni usafiri kwa daladala kwa sababu ni nafuu na hana unaweza kujua watu wengi na kuzungumza nao wao*
> *Jambo jengine ninalopenda kwamba hapa Unguja na Pemba wafanya biashara wanauza vitu wageni kwa bei juu au watu wengine hufuata watalii mitaani.*
> *Hapa chakula ni chali ni tofauti na nchi yangu kuna viungo vingi kama tangawizi, manjano na kadhalika.*
> Ninapenda sana fukwe nyeupe na bahari safi iliyojaa samaki.

Kipande hiki hakina ushikamani wa sentensi, maana, na mtiririko wa urejeleaji kwa sababu sentensi zinatoka mada moja hadi nyingine bila uhusiano wowote. Mawazo yanaruka bila mpangilio, na hakuna muktadha au muundo unaoeleweka kati ya sentensi.

Jina la mwanafunzi X, Y na Z yamebuniwa ili kufuata maadili ya utafiti ya kuficha usiri katika majina ya wanafunzi. Mifano mitatu iliyobainishwa hapo ni mwelekeo wa kukosa ushikamani. Maandishi hayo yamekosa ushikamani wa kimaana, sentensi, urejeleaji na ushikamani wa sentensi. Sentensi moja inaachana na sentensi nyingine.

Mshikamano wa kisarufi ni ile hali ya kushikana kwa sentensi katika matini kupitia vijenzi vya urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji wa elementi mbalimbali katika matini ili kuleta muwala na maana. **[3]** wanadai kwamba dhana ya mshikamano ni ya kipragmatik na hurejelea uhusiano wa moja kwa moja wa maana ndani ya matini fulani na kwamba mshikamano hutokea pale ambapo ufafanuzi wa elementi moja katika matini hutegemea ile nyengine. Dhana hii hujishughulisha na kipengele cha matini kinachobeba maana katika lugha. Matini huweza kuwa neno moja au sentensi moja au msururu wa sentensi. Mtiririko huo hujitokeza katika matumizi ya lugha. Kwa mwanafunzi wa kiswahili kwa wageni mtiririko huo hutokea pindi akiwa anamudu vyema umilisi wa lugha katika stadi zote za lugha kwa ufanisi.

3.4 Matumizi ya Msamiati

Msamiati ni jumla ya maneno yatumikayo katika lugha. Kila lugha ina misamiati yake na utaraibu wa kuzingatia katika utumiaji wa misamiati hiyo. Kiswahili kina utaratibu wa matumizi ya maneno yake pia. Utaratibu huo hupaswa kuzingatia muktadha sahihi wa matumizi, uandishi fasaha na sanifu wa maneno. Makosa ya msamiati ni hali ya mtu kutumia neno moja kinyume na neno hilo. Makosa hayo yanaweza kujitokeza kwa kutumika neno sehemu ambayo sio yake na kudhani kuwa ni sahihi. Ingawa kwa wageni wanaojifunza Kiswahili makosa ya msamati hayajitokezi kwa namna hiyo bali yamegunduliwa katika kuhamisha tafsiri ya lugha zao na kuleta kwenye lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, neno mpunga, na wali katika lugha ya Kiswahili ni maneno tofauti lakini wanafunzi wanaojifunza Kiswahili wameyafanya ni maneno sawa. Wanafunzi katika kutunga sentensi amesema **<John amepanda wali Pemba>** badala ya kusema **<John amepanda mpunga Pemba>** neno **<rice>** wamelichukua kwa dhana ile ile ya wali au mpunga ilihali katika lugha ya Kiswahili vitu hivyo huchukuliwa kwa dhana tofauti. Katika hali hii tunaona kuwa lugha hutegemeana na utamaduni wa jamii na utamaduni lugha kama ilivyo nadharia yetu. Hata hivyo, Nadharia ya umilisi wa lugha huwa inazingatia utamaduni lugha. Kwa hivyo, kukwepa utamaduni lugha ni kukosa umilisi wa lugha husika. Hali hiyo, ndiyo iliyotuongoza na kubaini kuwa mwanafunzi aliyesema amepanda mpunga pemba kuwa amekosa. Ingawa katika muktadha wa utamaduni wa lugha yake neno <**rice**> linaweza kuwa mpunga.

Sentensi nyingine ambayo imejitokeza kuwa na makosa ya msamiati ni neno pika na tengeneza. Mwanafunzi alipotakiwa atunge sentensi kuhusu chai alisema **< Genna ametengeneza chai kwa ajili ya wageni>** mwanafunzi mmoja 01 ametumia neno tengeneza badala ya kupika. Katika lugha ya kiswahili chai huwa haitengenezwi bali hupikwa. Hivyo neno tengeneza kujumuisha kwenye juice au vitu vingine lakini sio chai. Pia, wanafunzi walitatizika kwenye sentensi isemayo <**mkate imeokewa vizuri sana>** badala ya kusema <**mikate imeokwa vizuri sana>** wanafunzi wanne kati

ya wanafunzi watano walisema neno <**imeokewa>** sawa na asilimia 80% Hii ni wazi kuwa utumiaji wa msamiati mmoja katika utamaduni wa lugha moja unaweza kutofautiana na utamaduni wa lugha nyingine. Hivyo ni wazi kuwa wanafunzi wanashindwa kufuata kanuni za kisarufi wakati wa kuandika sentensi zao na pia wanashindwa kufahamu utamaduni lugha jamii jambo ambalo ni muhimu sana katika kujifunza lugha ya pili.

Vile vile kuna wanafunzi walisadifu kutumia neno pika katika chai ila limejitokeza kuwa na makosa katika kitenzi pika, kuwa kupika na badala yake majibu mengi ya wanafunzi yalikuwa <***chai kimepikwa***> na **<chai zimepikwa>** badala ya chai imepikwa.

Hivyo, kwa mujibu wa maelezo hayo mwalimu anayefundishwa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa wanafunzi wa kigeni anapaswa kusisitiza suala la utamaduni lugha kwa sababu katika Kiswahili hatupandi wali wala hatutengenezi chai. Hivyo, mwalimu anapaswa kudokeza suala hili wakati wa ufundishaji ili kuepusha makosa hayo. Aidha, katika lugha ya Kiswaahili ipo misamiati kadha inayowatatiza hata wazawa wa lugha. Kwa mfano, matumizi ya neno ukwasi na utajiri, mazingira na mazingara hutumiwa na watu wengi kimakosa. Hivyo, wazungumzaji wa lugha wanapaswa kuwa na umilisi mzuri wa kamili wa lugha na sio nusu nusu.

3.5 Ukanushi wa Vitu vya Karibu

Kutomudu ukanushi wa vitu vya karibu ni miongoni mwa makosa yaliyobainika kufanywa na wanafunzi wa kiswahili kwa wageni. Katika lugha ya Kiswahili sentensi inaweza kuwa na hali kadhaa zikiwemo ukanushi, mazowea na hali ya kawaida. Mwanafunzi wa lugha anapaswa kuwa na ufahamu kuhusu matumizi ya sentensi katika hali ya kawaida na hata katika ukanushi. Ukanushi wa karibu unahusisha kukanusha sehemu maalum ya sentensi, kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, au kipashio kingine chochote ndani ya sentensi. Ukanushi huu unaelekezwa kwenye neno au kipashio fulani ili kubainisha kwamba kipashio hicho pekee kinakanushwa, badala ya sentensi nzima.

Katika ukanushi wanafunzi wanaojifuza Kiswahili wameonekana kushindwa kumudu vizuri. Makosa mbalibmbali yamegundulika kujitokeza kwa wanafunzi wa Kiswahili kama lugha za kigeni ni kutomudu vizuri matumizi ya ukanushi hasa pale walipotunga sentensi kuhusu vitu. Kwa mfano katika sentensi **< *kijiko sinaanguka*>** wanafunzi wawili walishindwa kupeleka ukanushi katika viambishi vinavyo kubalika, wote walisema **<*kijiko sianguki*>.**

Pia katika sentensi hii mwanafunzi mmoja kati ya watano alitunga sentensi kwa kusema **< *kijiko sinaanguka*>** Kwa maelezo hayo wanafunzi wamejichanganya kati ya ukanushi wa nafsi na ukanusi katika sentensi unaotumia kitu kisicho nafsi. Pia, wanafunzi wameshindwa kugundua nafsi pamoja na njeo na ndio maana wakasema <***kijiko sinaanguka*>.** Hapa wanaonekana kutumia nafsi ya utendaji wa binaadamu kuliko kitu. Pia katika sentensi <chandarua kimechanika wanafunzi walishindwa kutumia ukanushi wanafunzi watatu kati ya watano walisema **<*chandarua sinachanika*>**

Kutokana na maelezo hayo ni Dhahiri wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa wageni wanaokabiliana na changamoto za ukanushi katika sentensi. Tatizo hili limezungumzwa na kujadiliwa na wataalamu mbali mbali. Kwa mfano, **[3]** anaunga mkono kwa kusema, Kuwa miongo kadhaa Chomsky amekuwa akifuatilia Sarufi ya lugha za Ulimwenguni (UG) katika jaribio lake

kueleza asili ya lugha na uhusiano kati ya lugha na akili. Pamoja na uzoefu wa lugha mama zinavyoweza kumuathiri mwanafunzi anayejifunza lugha ya kigeni, kwa maoni yake anasema ukanushi unaotumiwa na mwanafunzi huwa unazingatia lugha yake ya awali hivyo kusababisha makosa katika lugha ya kigeni**.**

3.6 Matumizi ya Viambishi Nafsi

[2] anaeleza nafsi ni kategoria ya kisarufi ambayo hudhihirisha mhusika katika tungo. Katika lugha ya Kiswahili kuna nafsi tatu ambazo hujitokeza katika maumbo ya umoja na wingi. Nafsi hizo ni nafsi ya kwanza ambayo huwakilishwa na “mimi” katika umoja na “sisi” katika wingi ambayo pia huwakilishwa na viambishi vipatanishi “ni” katika umoja na “tu” katika wingi. Nafsi nyingine ni nafsi ya pili ambayo huwakilishwa na “wewe” katika umoja na “nyinyi” katika wingi, ambayo pia huwakilishwa na viambishi vipatanishi “u” katika umoja na “wa” katika wingi. Nafsi ya tatu huwakilishwa na “yeye” katika umoja na “wao” katika wingi ambayo pia huwakilishwa na viambishi vipatanishi vya “a” katika umoja na “wa” katika wingi.

Viambishi nafsi ni jumla ya neno au maneno yanayorejelea nafsi ya mtenda au mtendwa jambo. Aidha, viambishi hivi huwa vinakaribiana utenda kazi wake na kazi ya upatanisho wa kisarufi. Lakini kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya kigeni walipimwa maswali ya kawaida na yenye urahisi katika kubainisha nafsi. Ila matokeo ya utafiti yanaonesha wanafunzi wengi kushindwa kumudu stadi hii ya uandishi.

Wanafunzi walitakiwa kuandika viambishi nafsi katika maneno kadhaa. Utafiti umebaini kuwa katika maneno hayo wanafunzi walishindwa kubainisha viambishi hivyo. Kwa mfano neno **<zunguka>** walipotakiwa kulitungia sentensi kwa kuliunganisha na neno mtoto. Wanafunzi watatu walisema **<mtoto kinazunguka>.** Pia, jina kipofu nalo liliwatatiza wanafunzi wanne 04 kati ya watano 05 walioshindwa kutumia kiambishi nafsi {a} kinachostahili kutumiwa katika kitenzi <-***mefika***>. Wanafunzi wengi waliofanya makosa walikuwa wakitoa jibu kama kipofu kimefika. Ingawa hapa tunaweza kuona kama ngeli lakini hapa walitakiwa kupachika nafsi katika neno **<*mefika*>** ndio maana wakatumia neno kimefika badala ya **<*amefika*>.** Kwa mujibu wa nadharia ya lugha ni matokeo ya utamaduni na saikolojia inaonesha wazi kuwa akili ya mzungumzaji huwa inakubali kuzungumza bila kuzingatia makosa hayo lakini utamaduni wa lugha ndio unabainisha kuwa kumetendeka kosa katika matumizi ya nafsi. Utafiti umegundua kuwa wanafunzi wengi wanaosoma Kiswahili kwa wgeni wanatumia sarufi ya lugha yao kuingiza katika lugha ya Kiswahil. Pia wanajumuisha katika uainishaji wa ngeli za majina hii wanafanya kwa sababu ya uzoefu.

3.7 Viambishi vya Umoja na Wingi

Viambishi ni vipashio au mofimu zinazowekwa kabla na baada ya mzizi wa neno. Viambishi vya nafsi pamoja na viambishi vya umoja na wingi huwa havizingatiwi mno kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Katika mawasiliano ya Kiswahili matumizi ya umoja na wingi hayatazamiwi kuwa ni makosa. Mfano, wanafunzi wamesikika wakisema **< yeye kuja hapa mapema>** au wengine husema **<wao mekuj hapa mapema>** kwa wingi, wakimaanisha **<yeye amekuja hapa mapema>** makosa hayo yameonekana yakivumiliwa kwa kiasi kikubwa na jamii

pamoja na walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wageni na hujipongeza kuwa wanafunzi wao wanajifundisha lugha kwa urahisi. Bali katika kuandika huonekana kuwa ndio makosa.

Kwa wanafunzi wanaojifundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni imekuwa kawaida kwa watumiaji wake kufanya makosa ya maumbo ya umoja na wingi. Mara nyingi hali hii hutokea pale ambapo maneno hupewa maumbo ya umoja na wingi isivyosahihi au kutopewa maumbo hayo hali yakihitajika au maumbo hayo kuchanganywa. Data zilionesha wanafunzi wanne 04 kati ya watano 05 wanakabiliwa na kosa hili. Neno saa limetumiwa kimakosa na kuwa masaa. Neno ofisi wamelitumia kwa wingi kuwa maofisini. Na pia neno udhaifu limetumika kuwa madhaifu. Makosa ya umoja na wingi yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili ni urahisi wa kupachika mofu {ma} katika mzizi kila mzizi wa nomino kama vile{saa} ili kudokeza dhana ya wingi wa saa. Hili ni kosa kwa kuwa **<saa>** ni mzizi huru ambao haupokei kiambishi chochote cha umoja wala wingi. Hata hivyo, makosa haya yanaonekana kufanywa na baadhi ya wenyeji wa lugha ya Kiswahili na ndio maana imeathiri wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili.

3.8 Hitimisho na Mapendekezo

Katika utafiti wa uandishi wa Makala haya kumejitokeza makosa mengi ya kuandika. Ufafanuzi zaidi unaonekana hapo chini.



jedweli linatuonesha kiwango cha wanafunzi kumudu stadi ya kuandika na kujitokeza kwa makosa kadhaa kama yalivyofafanuliwa hapo juu. Kwa mfano wanafunzi wawili 2/5 wamemudu kuandika kwa asilimia themanini 80%, pia wanafunzi wawili 2/5 wamemudu kwa asilimia 60% na mwanafunzi 1/5 amemudu kwa asilimia themanini na mbili 82. Ukichunguza asilimia hizo utabaini kuwa stadi ya kuandika imekuwa na ugumu kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni. Ingawa hali hiyo inachukuliwa kutia moyo na kuridhisha kidogo hata kama kumekuwa na makosa.

Matokeo ya utafiti wa Makala hii yanaonesha kuwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni bado wanakabiliwa na changamoto katika stadi ya kuandika, licha ya baadhi yao kuonesha kiwango cha kuridhisha cha umahiri kati ya asilimia 60–82. Hali hii inaashiria kuwa uandishi bado ni eneo gumu linalohitaji mkazo zaidi, hasa ikizingatiwa uwepo wa makosa mbalimbali ya kisarufi, na kimofolojia. Ili kuwasaidia wanafunzi, ni muhimu wahimizwe kuongeza mazoezi ya kuandika, kusoma maandishi mbalimbali ili kupanua msamiati wa kutosha na uzoefu wao wa kuandika.
Kwa upande wa walimu, kunahitajika mbinu shirikishi na bunifu katika ufundishaji wa uandishi, ikiwemo kuwafanyisha mazoezi ya mara kwa mara katika uuandishi kwa kazi za mtu mmoja mmoja au kazi za makundi, na kuunganisha teknolojia katika mazoezi ya kuandika. Walimu wanapaswa pia kuandaa masomo mahsusi yanayolenga makosa ya mara kwa mara ili kuwawezesha wanafunzi kujenga uwezo wa kuandika kwa usahihi na ufasaha. Mazingira chanya ya ujifunzaji, ambayo

yanawatia moyo wanafunzi na kupunguza hofu ya kufanya makosa, ni muhimu katika kuongeza kujiamini na motisha ya kujifunza.

Watafiti kwa upande wao wana wajibu wa kuchunguza kwa kina aina na chanzo cha makosa ya wanafunzi kupitia uchambuzi wa makosa. Utafiti zaidi unahitajika ili kubaini mbinu bora za kufundishia stadi ya kuandika, pamoja na kutengeneza zana za upimaji zilizo sahihi na rafiki kwa mwanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya pili. Aidha, utafiti kuhusu athari za motisha, mazingira ya ujifunzaji na ushawishi wa lugha ya kwanza utatoa mwanga mpana zaidi juu ya namna ya kuinua kiwango cha uandishi kwa wanafunzi hawa.

Marejeo

[1] Alamri, H. R. (2019). Writing proficiency levels among Arabic and English language student teachers and their perceptions of challenges in writing skill. *Journal of Literature, Language and Linguistics*, *62*(07), 62–75.

[2] Ali, L. H. (2015). Changamoto na mbinu za kiisimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa elimu ya awali. *(Unpublished master's thesis)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

[3] Flower, L., & Hayes, J. R. (1981). A cognitive process theory of writing. College Composition and Communication, 32(4), 365–387.

[4] Graves, D. H. (1983). *Writing: Teachers and children at work*. Heinemann.

[5] Halliday, M. A., & Hassan, A. (1976). *Cohesion in English*. Longman.

[6] Hyland, K. (2003). Second language writing. Cambridge University Press.

[7] Lehmann, C. (2006). *Linguistic competence*. Erfurt: University of Erfurt Publisher.

[8] Norrish, J. (1983). *Language learners and their errors*. Macmillan Press.

[9] Ogalo, M. (2011). Teaching techniques that enhance integration in the development of English language skills in secondary schools in Gatundu District. *(Unpublished master's thesis)*. Kenyatta University.

[10] Rivers, W. (2000). *Interactive language teaching*. Cambridge University Press.

[11] Sebazungu, P., & Ikuramutse, M. H. (2023). Factors leading to Kiswahili poor speaking skills in Kicukiro secondary schools, Rwanda. *Journal of Research Innovation and Implication in Education*, *7*(2), 61–68.

[12] Verah, M. K. (2017). Factors affecting students' acquisition of speaking skills in English among secondary schools in Turkana East District, Kenya. *(Unpublished master's thesis)*. Kenyatta University.

[13] Zahir, C. A., & Zannat, M. (2021). Barriers to teaching English productive skills in online classrooms: A study at private universities in Bangladesh. *International Journal of Linguistics, Literature and Translation*, *4*(12), 164–171.